

THE STATE UNIVERSITY  
OF ZANZIBAR  
P.O. Box 146  
Tel: 255-242230724/2233337  
Zanzibar – Tanzania  
Fax: 255-24-2233337  
E-mail: [vc@suza.ac.tz](mailto:vc@suza.ac.tz)  
Web site: [www.suza.ac.tz](http://www.suza.ac.tz)



CHUO KIKUU CHA TAIFA  
CHA ZANZIBAR  
S.L.P 146  
Simu: 255-24-2230724/2233337  
Zanzibar - Tanzania  
Fax: 255-24-2233337  
E-mail : [vc@suza.ac.tz](mailto:vc@suza.ac.tz)  
Web site: [www.suza.ac.tz](http://www.suza.ac.tz)

19 Machi, 2020

**TANGAZO KWA WANAJUMUIYA WOTE WA CHUO KIKUU CHA TAIFA  
CHA ZANZIBAR (SUZA) KUHUSU KUAHIRISHWA KWA SHUGHULI ZOTE  
ZA MASOMO ILI KUJIKINGA NA VIRUSI VYA COVID-19 (CORONA)**

Kutokana na agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed la kuzifunga skuli zote za Maandalizi, Msingi, Sekondari, **Vyuo Vikuu** na Madrasa kwa lengo la kupunguza uwezekano wa maambukizi ya maradhi ya *Covid-19 (Corona)* Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeahirisha shughuli zote za masomo katika Kampasi zake zote kuanzia Alhamisi tarehe 19 Machi, 2020 hadi hapo itakapotolewa taarifa nyingine kuhusu ufunguaji wa Chuo.

Kwa taarifa hii SUZA inaagiza ifuatavyo:

1. Mitihani yote ambayo haijafanyika na ilikuwa katika muendelezo wa kufanyika isimamishwe mara moja.
2. Wanafunzi wote wanaoishi katika dakhalia (*hostels*) za Chuo katika Kampasi zote zenye huduma hiyo wafanye maandalizi ya kuondoka haraka ndani ya dakhalia hizi.
3. Waajiriwa wote Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar waendeleo kuhudhuria kazini katika maeneo yao bila kuhusisha shughuli za usomeshaji wanafunzi hadi hapo itakapoagizwa vinginevyo.

Wanajumuiya wote wanaagizwa kuchukuwa tahadhari na kufuata maagizo yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na Serikali pamoja na wataalamu wa afya kuhusiana na kujikinga na uwezekano wa maambukizi ya maradhi haya thakili.

Dkt. Zakia Mohammed Abubakar  
**Makamu Mkuu wa Chuo**